Judgment and Mercy

# HUKUMU NA REHEMA

NA

DAVID B. WARD

**Chapishwa na:**
**United Pentecostal Church of Tanzania**
**SLP 1271**
**Moshi, Tanzania**

**REHEMA NA HUKUMU NITAZIIMBA EE BWANA NITAKUIMBIA ZABURI.**
**ZABURI 101:1**

Ni muhimu kwetu kuona rehema na hukumu vikifanya kazi mkono kwa mkono katika mpango wa Mungu. Mawazo haya lazima yaonekane kuwa yanafanya kazi pamoja na wala hayapingani. Rehema siku zote hupatikana ijapokuwa haiondoi hukumu, zaidi, hukumu hulainishwa na rehema ili kuleta matokeo yaliyotamaniwa na Mungu. Utekelezaji wa matamanio ya Mungu katika mambo ya hukumu lazima yawe ya kwanza tuyape nafasi ya kwanza wakati wa kushughulika **na ndugu zetu watendao maovu.**

Bila shaka kuna korongo pande zote mbili za njia . Kutoa ushauri kuhusu mkosaji haina maana kuwa tutaweza kuruhusu dhambi ndani ya kanisa. Kutoa rehema kwa ndugu aliyeanguka haina maana kuwa hatujali au tunapendezwa na matendo yake. Kusudi ya rehema ni ili tuondoe ugonjwa ili kumwokoa mgonjwa, hatimaye kumrejesha katika maisha ya kiroho na afya kwa msaada wa Bwana mponyaji.

**KUPOTEA NA KUPATIKANA**:

Mfano pekee wa ndoa ya hukumu na rehema unaonekana katika maisha ya Hosea.

**NAMI NITAKUPOSA UWE WANGU KWA MILELE, NAAM NITAKUPOSA KWA HAKI, NA HUKUMU, NA KWA UFADHILI NA KWA REHEMA.**
**HOSEA 2:19**

Kwa amri ya Mungu, Hosea alichukua mke ambaye alikuwa kahaba (Hosea.1:2). Huu ungekuwa ni mfano kwa Israeli kutokuwa na uaminifu na pia ufafanuzi wa hukumu na rehema ya Mungu kwa watu wake.

Hosea akamtwaa Gomeri kama mke kuwa wake na kumpenda, akijua uovu wake wa nyuma na pia alitahadhari kuwa maisha yake ya zamani yanaweza kufufuliwa na kuongozwa katika kutokuwa mwaminifu. Kwa jinsi hiyo hiyo, Mungu anatupokea na kutukubali mwenyewe katika uwezekano wa kuumizwa na kukataliwa ambapo siku zote kunakuweko wakati tunapofungua moyo wetu kumpenda mtu.

Kwa Gomeri kutokuwa mwaminifu na kutafuta wapenzi wengine kulivunja moyo wa Hosea na kuuvunjilia mbali uhusiano wao kati ya mume na mke. Katika hatua hii Mungu alionyesha hukumu yake kwa kuondoa baraka na ulinzi kutoka kwa mdhambi. Hata hivyo, ifahamike kuwa hii haikufanywa kwa lengo la uharibifu, lakini zaidi ili aone hilo kosa la njia yake na arejeshwe katika haki.

**BASI KWA AJILI YA HAYO, ANGALIA, NITAZIBA NJIA YAKO KWA MIIBA, NAMI NITAFANYA KITALU JUU YAKE, ASIPATE KUYAONA MAPITO YAKE. NAYE ATAWAFUATIA WAPENZI WAKE, LAKINI HATAWAPATA, ATAWATAFUTA, LAKINI HATAWAONA, NDIPO ATAKAPOSEMA NITAKWENDA NIKAMRUDIE MUME WANGU WA KWANZA KWA MAANA HALI YANGU YA ZAMANI ILIKUWA NJEMA KULIKO HALI YANGU YA SASA.**
**HOSEA 2:6-7**

Katika aya hizi nyingine zinazo fuatia katika Hosea sura ya pili tunaona hukumu ya Mungu (mstari wa tisa mpaka wa kumi na tatu) kisha rehema ya Mungu katika kuirejesha

Israeli (mstari wa kumi na nne mpaka wa ishirini na tatu).  Hukumu ya Mungu inayoelezwa hapo ni dhahiri kwa madhumuni ya kusahihisha zaidi ya uharibifu.  Tunatumia kanuni ya jinsi hii wakati wa kuwasahihisha watoto wetu.  Iwe ni uhakika kuwa ni makusudi yetu wakati wa kushughulika na watoto wa Mungu.

Bila kukosea kuna gharama ya kulipa wakati mtoto wa Mungu anapokosa.  Makovu ya dhambi yanabakia kwa kitambo kirefu baada ya jeraha kupona.  Hata hivyo, thamani ya ukombozi wetu imelipwa.  Rehema ya Mungu ilimsababisha Hosea kwenda kumkomboa yule kahaba, akajichukulia pamoja na nadhiri uaminifu (Hosea 3:1-3). Huduma ya kanisa katika kumrejesha aliyeanguka kutubu na kurejea ni gharama  ambayo kwayo ndivyo rehema ya Mungu inavyotumika.

Hakika yote haya, hayana maana bila ya toba halisi ya walioanguka.  Toba ya Israeli katika Hosea sura ya sita ilitakiwa kwa ajili ya kurejeshwa kwao.  Hata hivyo hapawezi kuwa na urejesho wa Wakristo walioanguka bila kuziacha kando dhambi na kujiweka wakfu upya kwa Mungu.

Matokeo ya hayo yote katika kanisa ni ili tuwe waangalifu katika masamaha na urejesho wa aliyeanguka.

**BASI MRUDIE MUNGU WAKO, SHIKA FADHILI NA HUKUMU,**
**UMNGOJEE MUNGU WAKO DAIMA.**
**HOSEA 12:6.**

**MIMI NITAWAPONYA KURUDI NYUMA KWAO; NITAWAPENDA KWA UKUNJUFU WA MOYO, KWA MAANA HASIRA YANGU IMEMWACHA.**
**HOSEA 14:4.**

Mbinu hii tuchukie dhambi lakini tuonyesha upendo na rehema kwa mdhambi.

**BWANA WA MAJESHI AMESEMA HIVI, YA KWAMBA, FANYENI HUKUMU ZA KWELI, KILA MTU NA AMWONEE NDUGU YAKE REHEMA NA HURUMA.... WALA MTU AWAYE YOTE MIONGONI MWENU ASIWAZE MABAYA JUU YA NDUGU YAKE MOYONI MWAKE.**
**ZAKARIA 7:9-10**

Mbinu rahisi zaidi wakati wa kushughulika na dhambi ni kumruhusu mdhambi afe bila rehema.  Hii itaondoa dhambi kutoka duniani lakini itashindwa kutekeleza mapenzi ya Mungu.

Ni mapenzi yake kuwa kusiwe na hata mmoja atakayeangamia.  Maadamu kuna tumaini la toba na urejesho ni jukumu la kanisa na kila mtoto wa Mungu kusaidia walioanguka kupata njia yao kurudi kwa Mungu.

**KISASI:**

**ANGALIENI MTU AWAYE YOTE ASIMLIPE MWENZIWE MABAYA; BALI SIKU ZOTE LIFUATENI LILILO JEMA, NINYI KWA NINYI NA KWA WATU WOTE.**
**I WATHESALONIKE 5:15**

Wazo la kulipiza kisasi ni la zamani kama mtu mwenyewe na inapatikana katika kumbukumbu za maandiko ya awali. Kaini ambaye alimuua nduguye alikuwa anaogopa kulipizwa kisasio na wengine. Kwa hiyo Mungu akaweka alama juu yake ili wanadamu watahadharishwe wasimlipize kisasi dhidi yake (Mwanzo 4:14-15). Ushahidi zaidi wa ulipizaji wa kisasi ndani ya maisha ya binadamu unapatikana katika Sheria ya Musa. Hesabu 35:27 inazungumzia kwa mwenye kutwaa kisasi cha damu na mji wa makimbilio muhimu kwa kumwokoa mtu na kisasi. Hata hivyo, uwepo wa kisasi jinsi hiyo katika sheria hakutoi kibali cha kulipiza kisasi kwa Mkristo. Tunajua ya kuwa sheria haikuwa na uwezo wa kumkamamilisha binadamu (Waebrania.7:19), na sasa tuna njia bora zaidi (I Wakorintho.12:31).

Ukweli ni kuwa kisasi kipo katika uwezo wa Mungu na mamlaka yake. h.sisi hatujapewa mamlaka hayo.

**KISASI CHANGU MIMI, NA KULIPA WAKATI ITAKAPOTELEZA MIGUU YAO. KUMBUKUMBU LA TORATI 32:35**

Mungu amejichukulia kisasi kuwa ni nafasi yake na ukweli ametuelekeza kuachilia mbali jambo hilo.

**WAPENZI, MSIJILIPIZE KISASI, BALI IPISHENI GHADHABU YA MUNGU MAANA IMEANDIKWA, KISASI NI JUU YANGU MIMI, MIMI NITALIPA ANENA BWANA.**
**WARUMI 12:19**

Mtu anayepuuza maelekezo ya Mungu na kujilipizia kisasi mwenyewe anakosea katika sehemu mbali mbali. Kwanza, kwa sisi kulipiza kisasi ni kuiba kitu kilicho cha Mungu. Alisema kulipa kisasi ni juu yake. Na pia kulipiza kisasi ni kupinga amri itokayo kwa Mungu moja kwa moja. Ukweli, yule anayelipiza kisasi, kiuhakika anajiweka mwenyewe katika nafasi ya Mungu. Kulipiza kisasi sisi wenyewe, kutakuwa kunaonyesha kutokuwa na imani kwa Mungu kuwa anaweza kushughulikia jambo hilo. Yote haya ni dhambi.

Tunaweza kujitoa wenyewe kwa kusema kuwa hatujawahi kuwa na kosa la kulipiza kisasi. Hata hivyo jambo linaweza kuwa limefichika kuliko linavyoonekana mara ya kwanza. Kukataa kujumuika katika mambo ambayo siyo muhimu, kuharibu mienendo ya wengine, pia hata kushindwa kwetu kutoa msaada au kumlinda mtu kwa sababu ya tatizo lililoko yote ni kushindwa kuwa na upendo na inaweza kutumika kama njia ya kulipiza kisasi. Kiwango cha maandiko kwetu sisi ni kuwa tusishindwe katika mambo ya upendo. Hatutaweza kamwe kulipa kikamilifu deni la upendo tulilonalo kwake kutokana na upendo wake kwetu.

**MSIWIWE NA MTU CHOCHOTE, ISIPOKUWA KUPENDANA KWA MAANA AMPENDAYE MWENZAKE AMETIMIZA SHERIA.**
**WARUMI 13:8**

Mungu anataka tumwamini katika kulipiza kisasi. Daudi alisema hivyo alipowaona waovu wakistawi, ilikuwa ni vigumu kwake mpaka alipoenda kwenye nyumba ya Mungu pale alikumbuka kuwa kutakuwa na hukumu na kuwa wote watafanyiwa haki. Wakati Daudi alipoona mwisho wa waovu, muda wao ni mfupi wa kuwa na utajiri haukumsumbua.

Mahali pengine anasema kuwa tusiwe na wasiwasi kwa sababu ya watenda maovu. Alijifunza hekima hii alipopeleka matatizo yake na malakamiko kwa Bwana. Tusifikiri kuwa

Mungu haoni matendo ya watu waovu au kwamba ataruhusu matendo yao kutokuadhibiwa, haswa kama yanafanywa na mmoja wa watoto wake.  Jukumu letu ni kuamini mkono mkuu wa Mungu wetu, ambapo kisasi ndipo kilipo.

**WATU WASIOLIPA BAYA KWA BAYA, AU LAUMU KWA LAUMU, BALI WENYE KUBARIKI, KWA SABABU HAYO NDIYO MLIOITIWA ILI MRITHI BARAKA.**
**I PETRO 3:9**

**TENA IWENI WAFADHILI NINYI KWA NINYI, WENYE HURUMA, MKASAMEHEANE KAMA NA MUNGU KATIKA KRISTO ALIVYO WASAMEHE NINYI.**
**WAEFESO 4:32**

Kuna miongozo ya ki-Mungu ziliyorudiwarudiwa aliyoitoa Mungu katika maandiko kuhusu masamaha.  Neno la Mungu haliachi mashaka kuwa mtoto wa Mungu atarithi asili ya Mungu ya kusamehe.  Mungu hapendi tu sisi tusamehe bali anahitaji hilo.

**BASI KWA KUWA MMEKUWA WATEULE WA MUNGU, WATAKATIFU, WAPENDWAO, JIVIKENI MOYO WA REHEMA, UTU WEMA, UNYENYEKEVU, UPOLE UVUMILIVU, MKICHUKULIANA, NA KUSAMEHEANA, MTU AKIWA NA SABABU YA KUMLAUMU MWENZAKE; KAMA BWANA ALIVYOWASAMEHE NINYI, VIVYO HIVYO NA NINYI.  ZAIDI YA HAYO YOTE JIVIKENI UPENDO, NDIO KIFUNGO CHA UKAMILIFU.**
**WAKOLOSAI 3:12-13**

Agizo la kimaandiko la kusameha linaenda kinyume na asili ya kimwili.  Hatusamehi haraka makosa ya wengine, haswa kama tendo hilo limetujeruhi.  Hata hivyo, jambo la kusamehe lina matokeo zaidi na kufikilia zaidi kuliko huruma zetu binafsi kwa kutomlaumu au kumkosoa ndugu aliyekosa.  Uhusiano wetu binafsi na Mungu na maisha ya kiroho kanisani yanatokana na kufaulu au kushindwa kwetu katika nyanja za masamaha.

Badiliko moja la mara la msamaha au kutokusamehe ni furaha yetu katika Bwana. Ki-uhakik  ndugu yake mkubwa wa yule potevu wa mali hakuweza kuingia katika furaha ya toba na kurejeshwa kwake.  Alichukizwa na ukweli kuwa ndugu yake mdhambi alikubalika na kurejeshwa.  Furaha ya tukio hilo iliyonekana kumkwaza.  Neno la Mungu lasema kuwa kuna furaha kule mbinguni kwa mdhambi mmoja akitubu.  Kama hatuwezi kushiriki kwenye hii furaha basi sisi tuna hasara.  Kama furaha ya Bwana ni nguvu yetu, basi lazima kusamehe mdhambi aliyetubu na tushangilie pamoja naye.

Jambo jingine ambapo masamaha yanageuza sana ni katika maisha yetu ya maombi.

**NINYI, KILA MSIMAMAPO NA KUSALI SAMEHENI, MKIWA NA NENO JUU YA MTU, ILI NA BABA YENU ALIYE MBINGUNI AWASAMEHE NA NINYI MAKOSA YENU.  LAKINI KAMA NINYI HAMSAMEHI WALA BABA YENU ALIYE MBINGUNI HATAWASAMEHE NINYI MAKOSA YENU.**
**MARKO 11:25-26**

Hapa masamaha yanaamriwa kuwa ni muhimu katika maisha yetu ya maombi.  Kitu kingine ambacho kinaweza kutajwa ni imani yetu katika kupokea masamaha.  Je, haingekuwa vigumu kwetu kuamini msamaha wa Mungu kama sisi wenyewe tungekuwa hatuna asili,

wengi wameshindwa katika jambo hili la imani la msamaha. Ni huzuni kuwaona wale ambao Mungu ana hiari kuwapokea wakishindwa kuingia katika baraka zake kwa sababu hawawezi kujileta wenyewe katika kuamini kuwa amewasamehe kiukweli.

**BASI UKILETA SADAKA YAKO MADHABAHUNI, NA HUKU UKIKUMBUKA YA KUWA NDUGU YAKO ANA NENO JUU YAKO, IACHE SADAKA YAKO MBELE YA MADHABAHU UENDE ZAKO, UKAPATANE NA NDUGU YAKO, KISHA UPESI UTOE SADAKA YAKO. PATANA NA MSHITAKI WAKO UPESI, WAKATI UWAPO PAMOJA NAYE NJIANI, YULE MSHITAKI ASIJE AKAKUPELEKA KWA KADHI, NA KADHI AKAKUPELEKA KWA ASKARI, UKATUPWA GEREZANI.**
**MATHAYO 5:23-24**

Neno muhimu katika maandiko hapo juu ni kupatanisha "kwanza patanishwa". Kama tumetenda kosa kwa mtu fulani, Mungu wetu hapendi kutuona madhabahuni mpaka tuwe tumepatana na ndugu zetu. Hii inahusu toba na masamaha. Haiwezekani kupatana bila ya vipengele hivyo. Kwa hiyo tunaona kuwa siyo tu masamaha yetu, kwa wengine bali pia toba yetu na masamaha yao kwetu ndiyo yanageuza uhusiano wetu na Mungu. Msamaha hapa umechukuliwa kama ruzuku. Maandiko hayasemi "Nenda kwa ndugu yako na uone kama atakusamehe" Kama tukitubu na ndugu yetu akikataa kutusamehe, basi hakika ni tatizo lake, hata hivyo kutokusamehe kwake kutakuwa na madhara kwa kanisa nzima kwa ujumla. Siku hizi upendo unapindishwa na kukubaliwa na maana kwamba, "upendo unamaanisha kuwa huwezi kusema umekosea" Hii ni kosa, upendo wa kweli unashirikisha toba na masamaha.

**MTU AKISEMA NAMPENDA MUNGU, NAYE ANAMCHUKIA NDUGU YAKE, NI MWONGO, KWA MAANA ASIYEMPENDA NDUGU YAKE AMBAYE AMEMWONA, HAWEZI KUMPENDA MUNGU AMBAYE HAKUMWONA.**
**I YOHANA 4:20**

**HIVYO WATU WOTE WATATAMBUA YA KUWA NINYI MMEKUWA WANAFUNZI WANGU, MKIWA NA UPENDO NINYI KWA NINYI.**
**YOHANA 13:35**

**KUSAMEHE NA KUSAMEHEWA:**

Kila mmoja wetu ana umuhimu kuhusika na utoaji pia upokeaji wa masamaha. Biblia imefanya haya mambo mawili pamoja na kuwa na uhusiano usiovunjika, kama tunataka kusamehewa lazima pia tusamehe.

**UTUSAMEHE DENI ZETU, KAMA SISI NASI TUWASAMEHEAVYO WADENI WETU.**
**MATHAYO 6:12**

**UTUSAMEHE DHAMBI ZETU KWA KUWA SISI NASI TUNAMSAMEHE KILA TUMWIAYE.**
**LUKA 11:4**

**KWA MAANA MKIWASAMEHE WATU MAKOSA YAO, NA BABA YENU WA MBINGUNI ATAWASAMEHE NINYI, BALI MSIPOWASAMEHE WATU MAKOSA YAO WALA BABA YENU HATAWASAMEHE NINYI MAKOSA YENU.**
**MATHAYO 6:14-15**

**BASI, IWENI NA HURUMA, KAMA BABA YENU ALIVYO NA HURUMA MSIHUKUMU NANYI HAMTAHUKUMIWA, MSILAUMU NANYI HAMTALAUMIWA ACHILIENI NANYI MTAACHIWA.**
**LUKA 6:36-37**

Yote haya yanaonyeshwa wazi katika ule mfano wa wadeni wawili (Mathayo 18:23-35). Kilio cha uchungu ili kuhurumiwa kilifanywa na mdeni wa mwanza ambapo kilizawadiwa na masamaha. Alisamehewa deni la talanta elfu kumi. Baadaye alimwona mtumishi mwenzake aliyekuwa anamdai talanta mia moja. Wakati alipodai kulipwa, mtumishi mwenzake alimwomba amsamehe kama alivyofanyiwa yeye. Hata hivyo, hakumsamehe na alimtupa yule mtu gerezani. Wakati mfalme aliposikia haya, alifutilia mbali ule msamaha aliokuwa amempa yule mdeni asiyesamehe na alimtupa gerezani. Baada ya jambo hili na kwamba kama tunashindwa kusamehe baada ya sisi kusamehewa tutakuwa katika hatari ya kupoteza masamaha yetu.

**NDIVYO NA BABA YANGU WA MBINGUNI ATAKAVYOWATENDA NINYI MSIPOSAMEHE KWA MIOYO YENU KILA MTU NA MAKOSA YA NDUGU YAKE.**
**MATHAYO 18:35**

Hii inafanya gharama ya kuwa na kinyongo isiwe na mwisho na ya milele a kuendelea mbele na umilele.

**NDUGU MSINUNG'UNIKIANE, MSIJE MKAHUKUMIWA, ANGALIENI, MWAMUZI AMESIMAMA MBELE YA MLANGO.**
**YAKOBO 5:9**

Hatuwezi pia kuwa na uamuzi wenye nguvu wa kiwango cha kusamehe. Wakati Luka 17:4 anasema ni lazima tusamehe mtu mara saba katika siku moja kama inawezekana. Mathayo 18:22 anaonyesha idadi ya sabini mara saba. Hakuna hata idadi moja imetolewa kuonyesha kiwango cha huruma na masamaha yetu, lakini kuonyesha ukuu wake.

Wakolosai 2:13 inaonyesha kuwa Mungu ameshasamehe makosa yetu yote kama tutakuwa kama Kristo, basi lazima tumfuate katika hali ya masamaha.

## BARAKA KATIKA KUSAMEHE:

Ninaweza kukumbuka miaka iliyopita katika mwanzo wa uchungaji angu, jinsi Mungu alivyonifundisha baraka katika kusamehe. Fedha zilikuwa haba. Hatukuweza kutembelea familia yetu kwa njia ambayo tungefanya kwa kuwa ilikuwa safari ya gharama ya maili kadhaa. Wakati mwinjilisti fulani na mke wake walikuwa wanaelekea njia hiyo na wakajitolea kumchukua mke wangu kutembelea familia yake, tulikuwa na uwezo wa kukusanya pesa kidogo kwa ajili ya nauli ya kurudi. Tulikuwa na furaha kwa kuweza kwake kwenda safari hiyo. Usiku wa kwanza alipokuwa ameondoka alinipigia simu. Wakati

wakisafiri walisimama ili kupumzika.  Wakati walipokuwa pale mtu mmoja aliiba kutoka katika pochi ya mke wangu pesa zote alizokuwa nazo wakati huo.

Hizi zilikuwa ni habari za kuchanganisha na usiku ule sikuweza kupata usingizi. Nilichoweza kufikiri tu ni jinsi inavyotisha kwa mtu kuiba kiasi kidogo cha fedha ambazo ni vigumu kuzipata.  Ninakiri kuwa hisia zangu hazikuwa ni za kusamehe, ninavyofikiria jinsi yule mwizi mwovu anavyostahili kuadhibiwa kama Mungu angemweka yule mtu katika mikono yangu wakati huo ninaogopa ningekuwa na hukumu ya kikatili sana.  Hisia zote hizo, hata hivyo, hazikumkamata yule mwizi, wala kumleta katika haki.  Jinsi ilivyotokea nilikuwa ni pekee niliyeathiriwa hisia zangu.  Jinsi hasira yangu ilivyokua na kukua nilijikuta mwenyewe kutopata usingizi.  Mwisho roho wa Mungu alinikemea.  Alinikumbusha kuwa nilipaswa kuwa katika shughuli za kuvuna roho, na siyo kufanya kama hakimu mwamuzi na mtendaji.  Pamoja na mkono mzito wa lawama juu yangu, niliondoka kitandani na kuanza kumwombea yule mwizi.  Kwanza nilimwomba Bwana anisamehe kwa kuhukumu na kisha nikamwomba Mungu amsamehe yule mwizi na amwongoze katika wokovu.  Wakati nikiwa katika kuomba, ule wasi wasi na hasira viliniondoka na roho mzuri mtamu akashika nafasi yangu.  Kisha nikaenda kitandani na moja kwa moja nikaishia usingizini. Hatukuwea kuzipata tena zile fedha, lakini Mungu alishughulikia mahitaji yetu.  Hatukumshika yule mwizi, lakini sikupoteza tena usingizi kuhusu swala hilo.  Tendo la msamaha limeondoa mateso yaliyosababishwa na matendo maovu, na amani na furaha vikapewa nafasi yake.

Siyo mapenzi ya Mungu kwa sisi kushindwa katika masamaha.  Kinyongo na uadui vinahuzunisha roho wa Mungu.

**MSIMHUZUNISHE YULE ROHO MTAKATIFU WA MUNGU AMBAYE KWA YEYE MLITIWA MUHURI HATA SIKU YA UKOMBOZI.  UCHUNGU WOTE NA GHADHABU NA HASIRA NA KELELE NA MATUKANO YAONDOKE KWENU PAMOJA NA KILA NAMNA YA UBAYA TENA IWENI WAFADHILI NINYI KWA NINYI WENYE HURUMA, MKASAMEHEANE NINYI.**
**WAEFESO  4:30-32**

Shetani atajitahidi kutushawishi kuwa yote haya siyo haki.  Atajaribu kutufanya tutende kulingana na hekima ya kibinadamu. Kama tukijaribiwa kwa njia hiyo, labda itakuwa ni vyema kukumbuka kwenye shimo lile tulilochimbiwa.Hekima ya kibinadamu inatuweka pale.  Tunaweza tusielewe siku zote njia ambayo Mungu anavyotuongoza,  lakini kama tukilinganisha maisha yetu kabla na baada ya kuanza kuishi kufanya mambo katika njia ya Mungu, itatusaidia sisi kudumu kwenye mwelekeo sahihi

Ayubu alikuwa na haki.  Alikuwa anatembea katika kumpendeza Mungu, alijua kwamba matatizo yake haikuwa adhabu ya Mungu.  Vigumu jinsi ilivyokuwa kuchukuana na huzuni yake, hasara na ugonjwa wake, haikuwa rahisi kuendana na wale "wafariji" watatu ambao walikuja katika njia yake na kumshitaki.  Walimlaumu na kumshitaki Ayubu mara kwa mara mpaka akachanganyikiwa na kujisikia kushindwa.

Wakati alipokuwa akijaribu kutafuta kuwa Mungu yuko wapi, kushughulika na mke mwenye kashifa, hasara zake, na kukuna majipu yake, hawa washitaki watatu hawakuacha kumshitaki.  Hatimaye, majaribu ya Ayubu yalifikia mwisho.  Unaweza kubuni nini ambacho angefanya?  Hasira ya Mungu ilikuwa juu ya wale wafariji watatu na aliwaambia watoe sadaka ya kuteketeza kwa makosa yao.

**KISHA BWANA AKAWAAMBIA NJIA PEKEE YA YEYE KUIKUBALI SADAKA YAO NI KAMA AYUBU ATAWAOMBEA.**
**AYUBU 42:7-9**

Zaidi ya hapo mateso yao yangeonekana ya kawaida kama Ayubu angekataa kuwasaidia. Hata hivyo, Ayubu alikuwa mtu wa haki. Alifanya kile kilichokuwa haki bila kujali hisia zake. Sasa angalia nini kilimtokea Ayubu wakati alipokuwa na rehema.

**KISHA BWANA AKAGEUZA UTEKA WA AYUBU, HAPO ALIPOWAOMBEA RAFIKI ZAKE. BWANA NAYE AKAMPA AYUBU MARA MBILI KULIKO HAYO ALIYOKUWA NAYO KWANZA.**
**AYUBU 42:10**

Mara nyingine shetani anajaribu kutuambia kuwa Mungu hayuko sahihi, kwamba hiyo haifai kusamehe. Ninafikiri unaweza kukumbuka Ayubu 42:10.

Kutokana na yote haya tunaweza tukamalizia kuwa masamaha yetu wenyewe, baraka za Mungu juu yetu kama binafsi na kama kanisa na amani na furaha ya Roho Mtakatifu katika maisha yetu vyote vimefungwa katika jambo la masamaha. Inawezekana makanisa kupata uamsho wanoutafuta pasipo kuondoa kumaliza vinyongo miongoni mwao na kujaribu kuwa na masahama? Pengine uponyaji wa mwili ambao baadhi wameutafuta unaweza kupokelewa baada ya kuacha kumhuzunisha Roho Mtakatifu na kuwa na masamaha toka ndani ya moyo. Kitu pekee tunachokipoteza wakati tukisamehe ni moyo mgumu na roho yenye uchungu masamaha yanalipa zaidi kuliko inavyogharimu.

**UNAPOSHINDWA KUSAMEHE**:

Sasa kushughulika na asili zetu za kimwili. Ni vyema na vizuri kuzungumza juu ya masamaha kutoka ndani ya moyo kama unaweza kutoa, lakini vipi kuhusu wakati ule moyo wako hautaki kusamehe? Inaweza kutokea kwa kila mtu na tunahitaji kujua la kufanya wakati hatuwezi kufikia hatua ya kusamehe. Kusema kiurahisi, kutoweza kusamehe ni kukosa upendo. Chuki, uchungu, na hata ukorofi ni matokeo ya asili wakati umekosewa. Bila kuweza kuepuka kutendewa vyema, basi lazima tujue jinsi ya kushughulika na kazi hizi za mwili.

Mashindano kati ya mwili na roho vinaelezewa vizuri na Paulo katika sura ya saba na ya nane ya kitabu cha Warumi. Adui wa tatizo hili ni akili za kimwili. Haimtii Mungu, ni adui wa Mungu. Kuwa na akili ya kimwili ni kufa kiroho. Kufikilia upendo ule unaoturuhusu kusamehe, lazima tushinde mawazo yetu ya kimwili.

Miongoni mwa mambo mengine, akili ya kimwili ina majivuno, choyo, uasi, na wivu. Kama tukiona wenyewe kuwa tuna jitahidi kumsamehe mtu, basi tuchunguze mioyo yetu wenyewe kwa ushuhuda wa kufikiri kimwili. Mfano pekee katika maandiko ya kushindwa kusamehe uko katika yule ndugu mkubwa aliyeshindwa kumsamehe nduguye mpotevu.

Kwanza kabisa tunamwona ndugu mkubwa akiwa shambani. Bila shaka alikuwa akifanya kazi kwa bidii na dhamira safi akitimiza jukumu lake. Jinsi alivyo karibia nyumbani alishangaa kusikia muziki na kucheza. Labda ghafula alikuwa na chuki kuwa haya yalikuwa yanatendeka wakati akifanya kazi shambani.

Haikuwa vyema kwa wengine kucheza wakati yeye alikuwa akifanya kazi shambani kwa bidii. Kisha alipotambua kuwa sherehe hizo zilikuwa ni kwa ajili ya ndugu yake asiyestahili, ilikuwa zaidi! kwa nini, hakustahili karamu kubwa namna hii, haikuwa sahihi. Alikuwa na hasira alipokumbuka dhuluma zote za nyuma. Kisha wakati baba yake alipokuja na kumsihi amsamehe nduguye na kushiriki katika karamu, alikuwa mwasi na kukumbuka makosa aliyoamini kuwa hakufanyiwa haki. Katika wivu, alikumbuka kuwa hakuwa amefanyiwa karamu yeyote, na alikumbuka dhambi zote za ndugu yake kama ushahidi wa upendeleo usiostahili wa baba yake.

Kwa hiyo tunaona jinsi akili ya kimwili ya ndugu mkubwa kulikozuia msamaha na kukubaliwa kwa nduguye anayetubu. Majivuno katika nafasi yake, choyo ambayo iliwachukiza wengine, uasi wakutokumsikia baba yake na wivu wa hisia kuwa hakuwa anatendewa haki kulizuia masamaha. Je, hii inasikika kuwa ya kawaida? Je, hisia za jinsi hii zimeshawahi kuingia katika miyo yetu mara kwa mara? Kama tunaweza kuelewa kwa uaminifu moyo wetu wenyewe wakati ni vigumu kusamehe basi tunaweza kutafuta sababu ya kushindwa kwetu. Hapa ndipo roho anaposaidia udhaifu wetu ikiwa tunasikia. Utendaji wa roho umeelezwa wazi katika Warumi sura ya nane. Kama tunaweza kuwa waaminifu na kumruhusu Roho afanye kazi ndani yetu, ushindi utakuwa wetu.

Hebu tuwe waaminifu kuruhusu uhuru wa Roho kufanya mapenzi ya Mungu ndani yetu na kuwa waaminifu wenyewe ni vitu ambavyo kila siku hatutekelezi. Hatukukamilika, na wakati mwingine hatuelewi faida kamili ya utoaji wa Mungu kwetu sisi katika Roho. Kuyaona makosa yetu hata kujua hisia zetu wenyewe inaweza kuwa vigumu kwa sababu yanaweza kufichwa ndani kabisa ya akili zetu.

**MOYO HUWA MGANDANYIFU KULIKO VITU VYOTE, UNA UGONJWA WA KUFISHA NANI AWEZAYE KUUJUA.**
**YEREMIA 17:9**

Sisi sote tumewahi ama wakati mwingine kutendewa vibaya. Wakati inapokuja kwa sisi kusamahe mtu fulani na inaonekana kutowezekana, tufanye nini? Vipi kama sielewi kwa usahihi au Roho hajapewa utawala? Hii imetolewa katika I Wakorintho 13:8 inasema kwamba ukiwapo unabii utabatilika, zikiwapo lugha zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika. Jibu la tatizo letu la kutokuweza kusamehe limetolewa katika sura hiyo hiyo. Upendo haushindwi.

Wakati fulani ilitokea kwangu. Nilijisikia kutotendewa vyema. Niliumia Nilikwazika. Jinsi nilivyo jua, nilikuwa nimemsamehe yule mkosaji na kila kitu kilikuwa sahihi. Hali zilivyo zilituchukua katika pande tofauti na tunaendelea na maisha yetu. Miezi ilipita bila kitu chochote kutokea na jambo lile likawa limesahaulika. Hata hivyo, moyo wangu ulinidanganya. Hisia ziliendelea kudumu ambazo sikuzijua kuwa zilikuwepo.

Nilikumbuka haya nilipomwona yule ndugu katika mkutano wa makambi. Hisia ziliinuka ndani ya moyo wangu ambazo zilinishtua na kuniogopesha. karibu ningegonga gari langu wakati nikiondoka toka uwanja wa makambi siku ile. Nilikuwa ninaogopa kukutana na yule ndugu na hisia hizi. Kufanya mambo kuwa magumu zaidi, nilisogelewa na mmoja wa viongozi wa jimbo siku hiyo hiyo. Alikuwa amepokea malalamiko kuhusu mtu huyo huyo na alitaka kuzungumza na mimi kuhusu yeye. Kama ningekuwa na nafasi ya kumshambulia mtu basi siku hiyo nilipewa. Jibu langu lilikuwa kwamba si kuwa na hakika kama nizungumze naye au hapana. Niliomba muda wa kuliombea. Usiku ule niliomba kwa bidii kupata kufunguliwa kutoka kwenye hisia zangu Nilimwomba Bwana anionyeshe nini sahihi na anisaidie kushinda kutokusamehe kwangu. Hakuna kitu kilichoonekana cha kusaidia. Karibu usiku mzima nilishindana na tatizo langu bila ya mafanikio. Mwisho nilimwomba

Mungu anionyeshe jinsi alivyokuwa akimwangalia yule mtu. Nilihisi kuwa kama ningeweza kuona jinsi gani Bwana anavyomwona ningeweza kujua nini cha kufanya. Ghafula nikawa na maono. Katika maono nilimwona yule mtu, hakuna zaidi . hata hivyo, nilivyomwona nilijihisi jinsi ninavyowaona watoto wangu. Watoto wangu wanakuwa na makosa yao, lakini ninawapenda hata hivyo kutoka wakati huo, tatizo langu lilitatuliwa. Ni miezi gani ya kutafuta akili yangu mwenyewe, na hisia na kujitahidi hakukunifaa, upendo ulikamilisha kwa muda mfupi.

Sasa Bwana hakunizuia mimi nisione makosa ya huyu mtu. Alinipa upendo ambao ni mkuu kuliko makosa na hisia. Tunaweza tukateswa na maumivu na kuumia kwa masiku, na miaka ya kupoteza furaha na ushindi. Tunaweza tukanaswa katika mtego wa kuamini kuwa hisia zetu ni sahihi na kufikiria kuhusu maumivu yetu mpaka yatawale maisha yetu yote. Tunaweza kuruhusu mizizi ya uchungu iote na kujilisha wenyewe matunda machungu. Au tunaweza kupenda.

**UPONYAJI KWA WALIOJERUHIWA:**

Sasa wengine wanaweza kuhisi kuwa wameumizwa mno kiasi cha kutopona, lakini lazima tukubali kuwa Mungu na upendo wake ni kubwa kuliko maumivu yoyote. Kuna mfano katika neno la Mungu ambao unatuonyesha njia ya kushughulika na maumivu haya. Inahusu Marko yule mtumishi, na mashaka yaliyohusu sikio lake.

**BASI SIMONI PETRO ALIKUWA NA UPANGA, AKAUFUTA AKAMPIGA MTUMWA WA KUHANI MKUU AKAMKAKTA SIKIO LA KUUME NA YULE MTUMWA JINA LAKE NI MARKO.**
**YOHANA 18:10-12**

Sasa nini? Hapa nimelala juu ya ardhi katika maumivu makubwa, maumivu yanayofanya vigumu kufikiri. Hata hivyo ni lazima nikifikiri kwa sababu ninao uchaguzi wa kufanya. Yule jamaa aliyetaka kujaribu kutwaa kichwa changu amesimama pale anaangalia kwa chuki kwamba ni sikio langu tu limelala chini na siyo kichwa changu. Ni mawazo mangapi yaliyokuwa yamepitia katika mawazo ya Malko alipokuwa amelala chini, akitokwa damu, akiwa ameshtuliwa na juu ya yote akiumwa kutokana na pigo la upanga wa Petro. Ni mara ngapi maumivu yanaweza kutuvuruga na kusababisha sisi kufanya makosa!

**DAWA YA ASILI:**

Mpige umlipizie jicho kwa jicho, au katika shauri hili, sikio! Malko angeweza kupigana na Petro na kutishia maisha yake zaidi ya yote alikuwa hapa akifanya kazi. Haikuwa inapendeza kupitapita kukamata wahalifu. Usiku angekuwa nyumbani akisheherekea pasaka na familia yake. Na sasa hii! Imeanza kwa maumivu, kisha kupotea sikio, pamoja na kuonekana vibaya siku zijazo na kuaibika, ndio alikuwa na kila haki ya kulipizia kisasi, au labda alifikiria hivyo.

**NJIA YA MWOGA KUJIONDOA:**

Maskini mimi! Sistahili hili hata kidogo! Tena akili inaweza kugeuka katika mawazo yake yenyewe. Marko angewageukia mashahidi waliokuwa kando yake na kujitetea dhidi ya mtenda kosa, anayependa kujinufaisha amtwae Petro. Alikuwa na shauri kamili Damu ilivuja na alilemaa, angeweza kuwasababisha wengine wamsikitikie kama angetaka, haswa kwa wale waliokuwa wanampenda. Marko angeweza kuendelea kufikiria juu ya hisia zake za

mauti na haki ya binafsi kwa miaka. Angeweza kuruhusu uchungu na kukua na angeweza kusimamisha kukua kwake kiroho na furaha, hata kuharibu maisha yake ya kiroho. Hicho ndicho Marko angeweza kufanya.

**TATIZO LIMETATULIWA:**

Pamoja na uchaguzi huu kwa nafasi ya kwanza katika akili yake Malko alikuja juu ya jingine. Pamoja na kutokuwa na kitu cha kufaidi isipokuwa kumjeruhi Petro, ambaye alikuwa mtumishi wa Mungu, kisasi kilionekana makosa sana, uharibifu sana kwa upande mwingine, kuishi ndani ya kujisikitikia kulionekana ni upotevu wa maisha yake mwenyewe.

Ndipo Malko akamtazama Yesu. Badala ya kuleta madhara kwa Petro au yeye mwenyewe, aliamua kulala pale na kumwacha Yesu amponye. Hicho ndicho Malko alichofanya, na hilo bado ni jibu la tatizo la kuumizwa na maumivu.

Wakati mwingine, mahali fulani kuna uwezekano kuwa ni mtu mzuri atakuumiza. Kwa kipindi kifupi cha kutokuelewa au hasira vitakugusa, hisia zinafanya vizuri.

Petro akauweka upanga wake na kulichukua neno la Mungu. Petro bila mashaka alikuwa mtu mzuri. Ooh Malko ulikuwa na busara sana, ulikuwa sahihi kumtazama Yesu mponyaji!

**HATUA SABA ZA MASAMAHA:**

Wakati tukiumizwa na makosa ya mtu, ni muhimu kwa kurejeshwa kwao kuwasamehe. Kutokuwasamehe kwaweza kuwazuia kujirekebisha kwao kufanya makosa.

Pia, ni muhimu kwa afya yetu ya kiroho kuweza kusamehe. Kuweka kinyongo kunasababisha uchungu, ambao baada ya muda unaenea katika akili zetu na kufanya kila tunachofanya kuwa kibaya. Ukombozi wetu kutoka kifungo cha kuumia kunategemea masamaha yetu kwa wale wanaotuumiza. Kanuni nzuri ya kujiwekea sisi wenyewe ni kwamba hatuna haki ya kukwazika .

**WANA AMANI NYINGI WAIPENDAO SHERIA YAKO, WALA HAWANA LA KUWAKWAZA.**
**ZABURI 119:165**

Kinachofuata ni mwongozo tu kutuongoza kupita hisia zetu za kuumizwa na jaribio la kulipiza kisasi na kufikia msamaha wa kweli. Tunaweza kuzitawala hisia zetu wenyewe na kujilazimisha wenyewe kufanya mambo haya. Mwili hautawaliki kwa haraka. lakini matumizi ya kanuni hizi za upendo zitatuongoza kwenye ushindi.

1. <u>Kutoa manufaa ya mashaka:</u>
   Ni asili kuwazia mabaya juu ya wengine. Hata hivyo, Biblia inasema kwamba upendo hupokea taarifa ya ubaya kwa pole pole na pia hauchukui makosa kwa urahisi.

**(HISANI) .....HAUGHADHABISHWI UPESI, HAUFIKIRI MAOVU.**
**I WAKORINTHO 13:5**

**NDUGU ZANGU WAPENZI, BASI KILA MTU NA AWE**

**MWEPESI WA KUSIKIA, BALI SI MWEPESI WA KUSEMA WALA KUKASIRIKA. YAKOBO 1:19**

Hakika kila mmoja wetu kwa wakati fulani amesababisha kuumia kwa mtu bila ya kukusudia kufanya hivyo. Katika hali ya namna hiyo tutaweza tu kuomba msamaha na kutegemea kuwa wameamini katika malengo yetu mazuri. Inawezekana sana kumwumiza mtu na wala usitambue. Katika shauri la jinsi hiyo, tegemeo pekee ni kuwa mtu aliyeumizwa atapokelewa katika roho ya rehema ili tuweze kupatanishwa na ndugu yetu. Kama ndugu na dada katika ufalme tutaamini kuwa hawajaribu kutudhuru. Kama Wafalme na Makuhani katika ulimwengu uliopotea lazima pia kufikisha rehema hii kwa watu ambao hawana.

Hii inamaanisha kuwa wakati mtu akiniumiza au kunikosea, kwamba jukumu langu litakuwa kuamini kuwa kosa hilo halikukusudiwa. Sasa hilo linaweza lisiwe wazo letu la kwanza. Hata hivyo, lazima liwe wazo muhimu mpaka lithibitishwe. Vinginevyo lazima tukumbuke ujumbe wa Zakaria.7:10 ambao unatuelekeza kuwa na rehema na kuwa kusiwe na mtu wa kuwazia baya dhidi ya ndugu. Mpaka tutakapokuwa na ukweli tutakuwa tunakisia tu. Hata hivyo katika sheria ya jinai, kukiweko na makusudi katika kosa linafikiriwa kwa makini sana. Pia hata mtu anafikiriwa kutokuwa na kosa mpaka athibitike kuwa ana hatia. Ni zaidi kiasi gani sisi kama watoto wa Mungu tutahiari kuwa na rehema katika hukumu na pia tuwe na hiari ya kuamini kuwa ndugu yetu hakuwa na kusudi la kutuumiza.

2. <u>Mwombee mkosaji</u>:

**LAKINI MIMI NAWAAMBIA WAPENDENI ADUI ZENU WAOMBEENI WANAOWAUDHI. MATHAYO 5:44**

Hii inaweza isiwe rahisi kufanya lakini kuwaombea wanaotuumiza kuna zawadi zake pekee. Kama tunaomba kwa moyo, tutajitahidi kuwa na mwenendo safi. Ni kinyume cha chuki na uchungu kumwombea mtu na kumwomba Mungu amsamehe na kuwabariki. Wengine watabisha kuwa hawawezi kiukweli kuomba maombi ya jinsi hiyo wakati wana hisia za kuumizwa au hasira dhidi ya ndugu zao. Hata hivyo, kuna kitu fulani kuhusu maombi yanayosaidia kuvunja vunja hisia hizo. Kama tukiomba maombi marefu, Mungu anasaidia maumivu yetu na kupona jinsi tunavyoendelea. Kumwombea mkosaji hatimaye hutusaidia sisi kumsamehe.

3. <u>Fanyeni mema kwa wale wanaowachukia</u>:

Tunarejea tena katika Matayo 5:44. Katika hatua hii ya kufanya vizuri kwa mkosaji tunasimama ili kufikiri juu ya kusamehe wengine na kuanza kufanya kwa kuwafanyia vyema, tunaanza masamaha kuwezekana. Inawezekana kumwombea mtu na bado kufanya usiwasiliane naye. Kitendo cha kufanya vizuri kwa mkosaji kinasaidia vikubwa sisi kuwasamahe. Mimi binafsi mineshaona mbinu hii ikitena kazi. Wakati mmoja kulikuwa na kutokuelewana kwangu na mchungaji mwingine. Maneno makali yaliyozungumzwa yalilegeza uhusiano wetu. Hatukua maadui wa kikweli, ila kwa kitambo hatukuwa na ushirika. Kisha siku moja nikaamua kuwa pameshachukua muda wa kutosha. Ilikuwa ni kipindi cha kipupwe na barafu nzito ilikuwa imeanguka. Nikiwa nimeweka beleshi katika gari langu. Niliendesha

kuelekea nyumbani kwake nikiwa na nia ya kwenda kukwangua barafu iliyoko njia ya kuingilia kwake na njia za pembeni pia.  Nilipofika pale njia hiyo ilikuwa safi, lakini kwa kuwa alikuwa nyumbani niliamua kumtembelea.

Alipogundua kuwa nilienda kumfanyia zuri, na tulikuwa na furaha ya kumtembelea ile chuki iliondoka.  Tatizo ambalo hakuna hata mmoja wetu hakulipenda, liliponywa kwa kufanya zuri.  Upatanisho unaweza ukazuiwa kwa sababu jamaa anajua kuwa amefanya baya na ana tatizo la kuamini kuwa umemsamehe.  Dhamiri yako nzuri katika kumfanyia jambo zuri itakuwa ushuhuda kwake kwamba umemsamehe.

Hii pia inafanana na Matayo 5:23-24 ambapo panaelekeza moja kwa moja kwenda kwa ndugu yule mwenye kitu dhidi yetu.  Ni dhahiri kutokana na maandiko haya kwamba Bwana anataka tukabiliane na tofauti zetu na kupatana.

Ni vigumu kitu kingine kugeuza vizuri zaidi hili zaidi ya kufanya zuri kwa ndugu aliyekosea.  Tena karibio hili laweza kufanywa hata kabla ya "hisia" ya masamaha kuwepo.  Kumfanyia zuri mtu itatusaidia kujihisi vizuri mbele zake.

**LAKINI ADUI YAKO AKIWA NA NJAA, MLISHE AKIWA NA KIU MNYWESHE, MAANA UFANYAPO HIVYO UTAMPALIA MAKAA YA MAWE KICHWANI PAKE.  USISHINDWE NA UBAYA, BALI UUSHINDE UBAYA KWA WEMA.**
**WARUMI  12:20-21**

4.  Endelea:

Tunazungumzia juu ya kuwa na tatizo katika kutoa masamaha.  Lazima tuwe macho kuwa hakuna hata moja ya hivyo vilivyotajwa kitaweza kufanya  kazi mara ya kwanza tu kufanya hivyo.  Ni katika kurudia rudia kanuni hizi za masamaha ambapo hatimaye tunapata ushindi dhidi ya mwili.  Usifanye kosa, kushindwa kusamehe ni kazi ya mwili, bila kujali sababu ambazo zitakuwa katika akili zetu.  Siku zote tunaweza kutafuta visingizio kwa kutokusamehe.  Kupata visingizio vya kumridhisha hakimu ni jambo jingine.

Katika kujadili juu ya masamaha Yesu aliulizwa ni mara ngapi inatakiwa kusamehe mtu.  Hii ilikuwa ni jaribio la kawaida la kibinadamu la kuweka mipaka ya upendo kwa ndugu na kuwajibika kwetu kwao.  Ile idadi ya saba ilipendekezwa na mwanafunzi kuwa ilikuwa ni kiwango kizuri kusamehe.  Yesu alikataa karibio hilo kwa kujibu sabini mara saba (Mathayo 18:21-22).  Kwa kuwa hakuna uwezekano wa mtu kukosea mara nyingi kiasi hicho, inawezekana kuwa Bwana hakutaka kuweka kiwango cha kusamehe.  Kwa vingine, alikuwa anasema kwamba hatuwezi kufuta deni letu la upendo, jukumu letu la kusamehe.

Faida ya kuendelea kusamehe, kumwombea ndugu yetu na kumfanyia vyema mara kwa mara kwa weza onekana kwa njia nyingine.  Ukweli ni kuwa kosa moja laweza kusamehewa mara nyingi.  Jinsi kosa litakavyokumbukwa, kila mara tunajaribiwa kukumbuka yale maumivu na kumshtaki ndugu yetu, halafu ni wakati wa kusamehe tena.  Nia hii, lengo kubwa la kusamehe tena na tena kama ni muhimu ndilo linazaa ushindi.

5. <u>Mtizame mkosaji kwa macho ya Mungu</u>

Je, wakati mtoto wako mdogo anapotambaa na kupanda juu ya mapaja yako kisha akakupa picha aliochora unafanya nini? Je unaangalia sanaa hiyo iliyochorwa kwa ufanisi mbaya na kumgombeza kwa sababu ya kutokuelewa ufundi? Au unamkumbatia vikubwa kumtia moyo kwa jaribio lake la kukufurahisha? Ukweli ni kuwa tunachukua furaha katika majaribio ya ovyo ya watoto wetu ya kutufurahisha. Inaonyesha upendo wao kwetu na hiyo ni muhimu sana kuliko ufanisi wao. Katika kuwaangalia watoto wetu tunaona wazi makosa yao lakini tunawapenda hata hivyo. Tunafanya kuwasahihisha na kuwapenda wakati huo huo.

Yule ndugu aliyeumiza hisia zako na kukukosea pia ni mtoto wa Mungu. Bwana anaona makosa yake na kushughulika kumsahihisha, lakini bila mashaka anampenda. Ukweli alikwenda Calivari ili aweze kusamehewa. Kama tutamtizama ndugu yetu na kumwona kupitia macho ya Mungu, masamaha haitakuwa vigumu.

6. <u>Tegemea toba yao</u>:

Ukweli kuwa mtu hajatubu haitupi haki ya kuweka kinyongo. Imani yetu ni kuwa toba yao itakuja, na masamaha yetu yanakwenda bila swali.

Lazima tumalize jambo la masamaha katika mioyo yetu wenyewe na mbele ya kiti cha enzi cha Mungu haraka mapema iwezekanavyo. Msamaha wa haraka unaleta uwezekano wa mapatano. Kama ni muhimu kwenda kwa huyu mtu ili kufanikisha mapatano, basi lazima tuende kutoa masamaha kwa upole. Kutoa masamaha kwa majivuno ni aina yake ya kulipiza kisasi. Nitasisitizia kuwa na imani kwa ndugu yangu. Sasa hivi anaweza akawa anashindana na mwili, lakini ninamtia moyo kushinda vita hivyo na kuweka msamaha tayari.

7. <u>Kubali wajibu wako kurejesha walioanguka</u>:

**NDUGU ZANGU, MTU AKIGHAFILIKA KATIKA KOSA LOLOTE,
NINYI MLIO WA ROHO MREJEZENI UPYA MTU KAMA HUYO
KWA ROHO YA UPOLE, UKIJIANGALIA NAFSI YAKO
USIJE UKAJARIBIWA WEWE MWENYEWE.
MCHUKULIANE MIZIGO NA KUITIMIZA SHERIA YA KRISTO.
WAGALATIA 6:1-2**

Masamaha haimaanishi kuwa tu wajinga kwa makosa ya mtu. Haimaanishi kuwa tunawaamini kabisa kuwa siku zijazo hatakuwa na kosa. Tumeitwa kuwarejesha walioanguka.

Ndugu yetu aliyeanguka hawezi kurejeshwa bila mapatano. Kukosa masamaha kunamzuia kurejea kwenye mwili, ambapo anaweza kuimarishwa na kulindwa.

Kukiwa na kuchunga dalili ambazo zaweza kuwa kupelekea mtego, mwingine tunaamini pamoja naye na kufanya kazi pamoja naye kwa ushindi kamili. Hapana, sisi siyo walinzi wa ndugu yetu. Sisi ni ndugu wa ndugu yetu. Kama inanibidi kuchukuana pamoja naye hadi atakapokuwa imara na uzima, ndicho tu nitumainicho kwake kunifanyia.

Kukubali wajibu wa kumrejesha ndugu yetu aliyeanguka inagharimu kuyatoa macho yetu kutoka maumivu yetu wenyewe na kumulika usikivu wetu juu ya baraka za kuleta uhai na afya katika sehemu ya mwili.

**NEEMA:**

**REHEMA NA KWELI ZISIFARAKANE NAWE; ZIFUNGE SHINGONI MWAKO ZIANDIKE JUU YA KIBAO CHA MOYO WAKO. NDIPO UTAKAPOPATA KIBALI NA AKILI NZURI, MBELE ZA MUNGU NA MBELE YA MWANADAMU.**
**MITHALI 3:3-4**

Rehema ya Mungu ni sehemu muhimu katika utaratibu wake.

Hakika wote lazima tutambue sehemu iliyo wazi ambapo rehema ya Mungu ilihusika katika wokovu wetu. Kwa sisi kuikubali rehema ya Mungu na kuwanyima wengine ni unafiki na ukatili. Sasa tunaishi katika nyakati za hatari. Ni muhimu kuwa tujiweke wasafi na huru kutoka doa la dhambi. Hivyo, hatuwezi kuruhusu juhudi zetu za usafi kuzuia utoaji wa rehema kwa wale ambao wanatubu kiukweli. lazima tuelewe kuwa na rehema kwa ndugu aliyeanguka siyo kinyume cha kujiweka wenyewe watakatifu.

**MAANA MUNGU HAKUMTUMA MWANA ULIMWENGUNI ILI AUHUKUMU ULIMWENGU, BALI ULIMWENGU UOKOLEWE KATIKA YEYE.**
**YOHANA 3:17**

Yesu alisema, "Mimi ndimi njia, na kweli na uzima...." Jinsi Ukweli ulivyofanyika mwili. Alitumwa hapa ulimwenguni ili kuleta rehema. Rehema ni sehemu ya kweli ambayo tumeshika kwa nguvu. Ukweli vyo vyote havitenganishwi mara kumi na mbili katika Agano la Kale rehema na ukweli vimeunganishwa pamoja katika aya iyo hiyo.

**KWA REHEMA NA KWELI UOVU KUSAFISHWA.**
**MITHALI 16:6**

Stefano na Yesu bila shaka ni mifano imara ya wazo hili la rehema. Wakati wa kuvumilia kitisho cha kusulubiwa Yesu alifundisha kusamehe. Stefano katika tendo lake la mwisho aliomba kwamba dhambi ya uuaji wa kikatili isihesabiwe.

Kwa maelezo, rehema ni "huruma" uvumilivu unaonyeshwa na mtu kwa mwingine (haswa mkosaji) ambaye yu katika nguvu zake na haonyeshi huruma" (Kamusi ya Oxford ya Kiingereza cha kisasa, chapisho la 6).

Kumbuka kuwa sababu yote ya kufanyika mwili na msalaba ni ili kuleta rehema. Hii siyo kusema kuwa tunapuuza dhambi. Upendo wa kweli na rehema kamwe haviwezi kupuuza dhambi katika maisha ya ndugu yetu. Rehema ni sehemu ya hatua ya kujitakasa na kurejea.

Katika siku moja wakati watu wanalinda "haki" zao kwa wivu tunatakiwa kuwa macho na tabia ya ukali na ukatili ya kumfikiria ndugu yetu aliyeanguka.

**KATIKA HILI TUMELIFAHAMU PENDO, KWA KUWA YEYE ALIYEUTOA UHAI WAKE KWA AJILI YETU IMETUPASA NA SISI KUUTOA UHAI**

**WETU KWA AJILI YA NDUGU.**
**I YOHANA 3:16**

Njia rahisi ya kumkaribia mkosaji ni kumpa kile anachostahili na kumalizana nalo. Kuonyesha rehema kunachukua muda, kuhusika binafsi pia tahadhari.

Vipi kama atarejea katika njia zake za dhambi? Je, hatutakuwa tumeshirikiana naye kwa kuwa tulikuwa "warahisi sana" katika kushughulika na makosa yake? Ni wangapi watakaotuambia, "Nilikuambia hivyo"? Tatizo la kumpa tu mkosaji lile analostahili bila ya kuwa na rehema ni kwamba, bila rehema hakuna hata mmoja atakayeokolewa. Pia, na katika kanuni ya maandiko tunategemea kutendewa sawa sawa na jinsi tunavyotenda wakati wa hukumu na rehema.

**BASI, IWENI NA HURUMA KAMA BABA YENU ALIVYO NA HURUMA. MSIHUKUMU, NANYI HAMTAHUKUMIWA, MSILAUMU NANYI HAMTALAUMIWA. ACHILIENI, NANYI MTAACHILIWA. WAPENI WATU VITU NANYI MTAPEWA KIPIMO CHA KUJAA NA KUSHINDILIWA, NA KUSUKWA SUKWA HATA KUMWAGIKA NDICHO WATU WAKACHOWAPA VIFUANI MWENU. KWA KUWA KILE KILE MPIMACHO NDICHO MTAKACHOPIMIWA.**
**LUKA 6:36-38**

Sasa, sehemu ya mwisho ya aya hiyo hapo juu mara nyingi hutumiwa katika baraka za Bwana kwa wale wanaotoa vitu. Hakuna mashaka kwa hilo. Hata hivyo shughuli hii ya "toeni nanyi mtapewa" imewekwa kati ya amri na rehema (mstari wa 36-37) na ile lawama ya kujaribu kuondoa kibanzi katika jicho la nduguyo wakati yetu yana boriti. Kama tunapenda kupokea rehema lazima tutoe rehema.

**MAANA HUKUMU HAINA HURUMA KWAKE YEYE ASIYEKUWA NA HURUMA. HURUMA HUJIKUZA JUU YA HUKUMU.**
**YAKOBO 2:13**

**BARAKA ZA REHEMA:**

Faida yetu katika kutoa rehema ni mbali kufikilia kwa mapana na ukubwa.. Kwanza kabisa inampendeza Mungu. Hakuna ushuhuda mkubwa zaidi katika kufanikiwa kwa mtu katika ufalme kuliko kusema kuwa amempendeza Mungu. Huu ulikuwa ushuhuda wa Henoko mwenyewe, alitembea na Mungu, na Mungu alipendezwa naye, na hali hiyo Henoko alinyakuliwa. Kisha kuna swala la rehema ya Mungu kwetu sisi. Biblia inazungumzia uhusiano maalum kati ya rehema tunazotoa na zile rehema tunazopokea. Matokeo ya kuwa na rehema kunageuza mienendo yetu na maisha ya kiroho. Mfano mzuri zaidi ni ule wa maisha ya Daudi.

**EE BWANA, MUNGU USIURUDISHE NYUMA USO WA MASIHI WAKO, UZIKUMBUKE FADHILI ZA DAUDI MTUMISHI WAKO. BASI SULEMANI ALIPOKWISHA KUOMBA MAOMBI HAYO, MOTO UKASHUKA KUTOKA MBINGUNI, UKATEKETEZA SADAKA YA KUTEKETEZWA NA DHABIHU, UTUKUFU WA BWANA UKAIJAZA NYUMBA.**
**2 MAMBO YA NYAKATI 6:42; 7:1**

Andiko lililonukuliwa hapo juu ni maneno yamwisho ya maombi ya Sulemani katika kuweka wakfu hekalu na matokeo ya mara kwa moja. Rehema za Mungu hazina ushuhuda zaidi kuliko katika maisha ya Daudi. Hatia ya uzinzi, uuaji na hila, Daudi bado alipata toba na urejesho.

Daudi aliitwa mtu wa moyoni wa Mungu mwenyewe. Licha ya matokeo ya kuhuzunisha ya dhambi yake, alibarikiwa vikubwa na rehema ya Mungu. Daudi aliamini rehema ya Mungu. hakuna shaka aliweza kufanya hivyo kwa kuwa alikuwa na rehema kwa wengine. Desturi hii ya rehema katika Daudi ilikuwa na mageuzi makubwa katika maisha yake na taifa la Israel kwa ujumla. Katika kitabu cha Isaya, wakati Bwana alipokuwa anaita Israeli kutubu, Ahadi yake ya masamaha zilirejea kwa rehema za Daudi.

**INAMISHA SIKIO LAKO, NA UJE KWANGU; SIKIA NA ROHO YAKO ITAISHI NAMI NITAFANYA AGANO LA MILELE NAWE, HATA REHEMA ZA KWELI ZA DAUDI.**
**ISAYA 55:3**

Kwa nini Daudi alipokea rehema nyingi kiasi hicho? sehemu ya sababu ni kwa kuwa na yeye alionyesha rehema kwa wengine. Rehema hizi zinaonyeshwa wakati Daudi alipokuwa akishughulika na Mfalme Sauli na nyumba yake.

Mara mbili (2 Samweli.sura ya 24 na 26) Daudi aliyahifadhi maisha ya mfalme Sauli. Katika matukio yote, Sauli alikuwa akimfukuza Daudi ili amuue. Katika kila kitambo, Sauli alitiwa katika mikono ya Daudi. Huruma za Daudi kumwokoa Sauli ni mfano wa kutisha juu ya rehema na upendo.

Wengi wangechukua upesi nafasi ya kumwangamiza adui, hata kuamini kuwa ni Mungu amekusudia. Ukweli ni kwamba mtu mwovu atajiangamiza mwenyewe. mtu mwema akiingia katika mtego wa dhambi anaweza kuja kwenye toba na kurejeshwa, kama akipewa nafasi. Hivyo ndivyo ilivyotokea zaidi ya mara moja katika maisha ya Daudi.

Mfano mwingine wa rehema katika maisha ya Daudi ni katika shauri la Mefiboshethi.
**KISHA DAUDI AKASEMA, JE! AMESALIA MTU MMOJA KATIKA NYUMBA YA SAULI NIPATE KUMTENDEA MEMA KWA AJILI YA YONATHANI.**
**2 SAMWELI 9:1**

Wakati huu Sauli na Yonathani walikuwa wamekufa na Daudi alikuwa kwenye enzi. Desturi za wakati ule ilikuwa kuangamiza yeyote katika nyumba ya ufalme uliopita ili wasiinuke dhidi ya mfalme mpya. Kinyume cha hiyo, Daudi akatafuta mpaka akamwona Mefibosheti na kumleta kutoka mbali, akamrejeshea urithi wake na akaribie meza ya mfalme.

Ni jinsi gani hii ilivyo kinyume na matendo ya udanganyifu ya baadhi ya "Wakristo" dhidi ya ndugu yao anayetenda dhambi. Uzuri wa hili ni kuwa Daudi hakumgojea Mefibosethi aje kwake na kumwomba msamaha. Rehema yake ilikuwa inamfikilia nduguye kumrejesha. Kwani ni muhimu kwa aliyeanguka kufanya hatua ya kwanza kuenda upatanisho, au tutachukua tahadhari na kutoa masamaha sisi wenyewe? Hivyo ndivyo Yesu alitufanyia sisi. Hiyo ndiyo rehema.

Inaweza kuonekana kuwa Daudi alionyesha rehema kwa sababu mbili, kwanza katika shauri la mfalme Sauli, alikataa kumgusa kwa sababu ya kumwogopa Mungu hangemgusa mpakwa mafuta wa Bwana. Pili, alimtafuta Mefiboshethi kwa sababu ya upendo wake kwa

Yonathani. Ingekuwa vizuri kwetu kuongozwa na kanuni hizo. Kumgusa mtoto wa Mungu, hata wakati yuko katika mtego wa dhambi, haimpendezi Mungu. Ila tu kama mtu huyo atakataa rehema ndipo anaweza kukataliwa na sisi. Hakika upendo ni sababu kubwa ya rehema. Haishangazi kuwa Daudi aliitwa mtu wa moyoni mwa Mungu mwenyewe.

**RIBA YA KIROHO:**

**NDIPO NIKAFANYA SHAURI RIBA YA KIROHO NA NAFSI YANGU, NIKAGOMBANA NA WAKUU NA MASHEHE NIKAWAAMBIA, MNATOZA WATU RIBA, KILA MTU NA NDUGU YAKE. NIKAKUTANISHA MKUTANO MKUBWA ILI KUSHINDANA NAO. NEHEMIA 5:7**

Kinyume cha rehema ni kuweka vizuizi katika njia ya kumrejesha ndugu. Kuhitaji zaidi kwa ndugu ambapo angehitaji ni kinyume na mahitaji ya upatanisho na kufanywa upya.

Wakati mateka walipokuja toka Babiloni kwenda Yerusalemu, walipewa baraka nyingi njiani. Kutokujiweza na kutokuwa na nguvu, Mungu aliwabariki na zaidi kutoka kwa mfalme. kuingia kwao Yerusalemu kuliwezeshwa kwa rehema za Mungu. Kila kitu walichokuwa nacho kiliwajia bure. Kwa hiyo, wakati walipohitaji riba kwa ndugu zao waliokuja baadaye, Mungu hakufurahi.

Kwanza, ilikuwa kinyume na sheria ya Mungu kwa Mwuisraeli kutoza riba kutoka kwa ndugu yake. Zaidi ya hapo, tuangalie tukio la haya kwa Nehemia sura ya tano. kwanza, tunaona kuwa ilikuwa wakope kutoka kwa ndugu zao chakula na kodi. Nyumba zao, nchi na mazao viliwekwa rehani katika njia hiyo. Kisha watoto wao walichukuliwa watumwa kwa sababu hawakuweza kulipa ndugu zao. Hii huwaadhiri watoto wetu na wengine katika kanisa wakati hatuki tayari kuwa na rehema ni uharibifu mkubwa.

**... KUMBE! TUNAWATIA UTUMWANI WANA WETU NA BINTI ZETU KUWA WATUMISHI... WALA HATUWEZI KUJIEPUSHA NA HAYO ILI KUWAKOMBOA. NEHEMIA 5:5**

Bila shaka swali tunawaleta watoto wetu na wote wanaotufuatilia katika utumwa wa kiroho wakati tunapoweka bei kwa kile tulichopata bure. Hii ni kutokuwa na riba ya kiroho.

Tulipookolewa, kuna mtu alituombea na kuchukua mzigo wa kutuleta kwenye ufalme. Kulikuwa hakuna gharama katika rehema na upendo huu. Kwa sisi, kujitukuza juu ya ndugu zetu ambao hawana nguvu kama sisi na kuhitaji wafanye zaidi kuliko uwezo wao, inafanana sana na njia ya Mafarisayo.

Wakati tukiwachukulia ndugu zetu hatua ya kutowakubali kwa majivuno kwa sababu ya udhaifu wao, tunasahau jinsi tulivyofika hapa tulipo. Bwana wetu anamtegemea kila mmoja wetu kukua katika neema na kuumbika katika mfano wake. hata hivyo anajua kwamba tunaanza kama watoto na uvumilivu kwetu ili kujitahidi.

Hatuwezi kulazimisha watu kukua zaidi kama vile tusivyoweza kulazimisha maua au mboga. Hadithi inasimuliwa ya mtoto aliyepanda mbegu za maua na kuchunguza jinsi yalivyopasua udongo pole pole na kukua. Kwa kutokuwa na uvumilivu jinsi mimea ile ilikua polepole, mawazo yakamjia ya kuyavuta kidogo ili yarefuke, akitegemea kuharakishe ukuaji

wake.  Alishitushwa asubuhi yake alipoona kuwa maua yale yalinyauka na kufa.  kwa kujaribu kusaidia alikuwa ameyang,oa,

Taratibu ya "wafanye walipe" wakati tunashughulika na ndugu aliyeanguka inalingana na kutokuwa  na hakika ya kiroho.  Matokeo ya dhambi ni ya kutisha na ya hakika.  Neno la Mungu linatuambia jinsi ya kushughulika na ndugu aliyeanguka.  Kufanya zaidi ya kile Mungu anachotuambia tufanye ni uhakika wa kutuelekeza katika kupotea.  Rehema inahitaji kumtafuta yule aliyeanguka, nafasi rahisi yao kutubu, na matokeo ya hiari na upendo.

Rehema ni pamoja na masamaha lakini inakwenda hatua moja zaidi mbele.  Wengine watakubali kusamehewa kama wakosaji watakuja kwao kuomba vinginevyo masamaha yatazuiwa.  Rehema inatafuta yule mkosaji na kumpa upendo, kufanya toba kuwezekane, na husamehe.  Rehema basi ni huruma na inasaidia wale dhaifu ili kuendelea.

Wakati rehema inapokataliwa, yule mkosaji anajizuia mwenyewe kutosamehewa na kuleta lawama juu yake mwenyewe.  hii haiwezi kusaidika, lakini hatujawa na hatia ya kutotoa rehema.  Mungu atusaidie sisi kujifunza rehema na kumpa aliyeanguka nafasi ya kuishi.

**NI UPENDO WA AINA GANI:**

**TAZAMENI, NI PENDO LA NAMNA GANI ALILOTUPA BABA.**
**I YOHANA  3:1**

Neno upendo limeshabadilishwa vya kutisha na kufanywa liovu kwa maana yake na watu wenye nguvu wa Hollywood na walimu wa Vyuo vikuu.  Kile kilichokuwa kinamaanisha kujitoa mhanga, kutenda wema na pia kujitoa dhabihu sasa lina maana ya raha, kujifurahisha na kuhusisha wengi kwa muda mfupi.

Hata katika matumizi ya maandiko, kwa maneno tofauti na maana tofauti hukusu upendo.  Upendo wa Mungu ni mkuu kuliko aina zote za upendo wa ulimwengu.  Upendo wake kwetu hauna mpaka, ni wa kujitoa dhabihu.na unatolewa bure.

**NAWE MPENDE BWANA MUNGU WAKO KWA MOYO WAKO WOTE, NA KWA ROHO YAKO YOTE, NA AKILI ZAKO ZOTE, NA KWA NGUVU ZAKO ZOTE... MPENDE JIRANI YAKO KAMA NAFSI YAKO.**
**MARKO  12:30-31**

Upendo wetu kwa Mungu na jirani ndio msingi wa sheria kama kanisa la Agano Jipya.  Baada ya kuwekwa kwamba Mungu wetu anatutaka tumpende binadamu mwenzetu, ni muhimu sana kwetu sisi    kutoa aina ya upendo ambao Mungu anakusudia.

**AMRI YANGU NDIYO HII, MPENDANE KAMA NILIVYOWAPENDA NINYI.**
**YOHANA  15:12**

Andiko hili moja linatukumbusha kwamba upendo wetu kwa wengine uwe kama Mungu alio nao kwetu.  Kuna hata mmoja amefikilia hilo?  Kama yupo, ni kwa sababu upendo wa Mungu unakaa ndani yake kupitia kazi za Roho Mtakatifu.  Kiwango cha juu cha kuwepo kwa binadamu ni kuishi na kufanya upendo kamili wa Mungu.

Muujiza wa wokovu wetu unategemea rehema na masamaha ya Mungu. Tunaburudika katika neema yake na kutegemea kutegemea yenyewe kwa ajili ya uzima wa milele. Tunampenda kwa sababu alitupenda kwanza. Na tuna mengi ya kufaidika katika uhusiano huu.

Jirani yetu anaweza asiwe na sifa zote za Mungu ambazo zitakufanya tumpende. Hata hivyo, tumeelekezwa kumpenda kama tunavyojipenda wenyewe, na kama Mungu alivyotupenda.

Sasa Mungu anatuona sisi kama watoto wake, na kutupenda licha ya makosa yetu. Anatusahihisha lakini anaendelea kutupenda katika njia hii tunaelekezwa kumpenda jirani yetu.

Upendo wetu kwetu wenyewe tunapewa licha ya makosa yetu. Ukweli mara zote tunaona makosa yetu pole pole. Haiwezekani tusijipende. Wengi wetu wanaona rahisi kidogo kusamehe, ambapo ni chanzo kikubwa cha amani. Katika kutuelekeza tuwapende wenzetu kama sisi wenyewe, Bwana ana tuamuru kuvumilia, masamaha yanayotolewa bure na amani.

Kama tutamruhusu Bwana afanye kazi ndani yetu kwa upendo huu, basi ndugu yetu aliyeanguka ana tumaini kurejeshwa.

**KUMREJESHA ALIYEANGUKA:**

**HUNIHUISHA NAFSI YANGU, NA KUNIONGOZA KATIKA NJIA ZA HAKI KWA AJILI YA JINA LAKE.**
**ZABURI 23:3**

Wote tunafurahia ridhaa ya Mungu kuturejesha. Kwa sababu ya utunzaji wake mwororo na uchungaji tunalishwa, tunaongozwa na kusaidiwa hata wakati tuko dhaifu au kuanza kupotoka. Kwa sababu mchungaji wetu anawapenda kondoo zake, tunaweza tukarejeshwa.

Huduma hii ya urejesho imepewa kanisa. Wakati ndugu na dada zetu wanapoanguka, ni wajibu wetu kuwafikilia na kutoa msaada, kuwatia moyo katika Bwana.

Jambo moja la muhimu katika huduma hii ni katika roho iliyotolewa. Rehema iliyotolewa katika mzaha wa kuaibisha siyo tu kukaribia kukataliwa, haipo katika mpango wa Mungu wa utekelezaji.

**NDUGU ZANGU, MTU AKIGHAFILIKA KATIKA KOSA LOLOTE, NINYI MLIO WA ROHO MREJESHENI UPYA MTU KAMA HUYO KWA ROHO YA UPOLE, UKIJIANGALIA NAFSI YAKO USIJE UKAJARIBIWA WEWE MWENYEWE.**
**WAGALATIA 6:1**

Mungu atupe viongozi na washirika wenye nguvu ya upole! Katika ulimwengu wa majivuno na uchoyo upole hupotea. Tumaini la huduma ya kurejesha hupotea bila upole.

**... MWENYE KUREHEMU, KWA FURAHA.**
**WARUMI 12:8**

Inakaribia kutokuwezekana kuficha roho yenye kinyongo. Juhudi yoyote ya kumrejesha ndugu yetu aliyeanguka isipofanywa kwa hiari na dhamiri safi ni dhahiri kushindwa. Kumbuka furaha ya baba wakati mwanaye mpotevu aliporudi.

**EE MWANADAMU, YEYE AMEKUONYESHA YALIYO MEMA NA BWANA ANATAKA NINI KWAKO, ILA KUTENDA HAKI NA KUPENDA REHEMA, NA KWENDA KWA UNYENYEKEVU NA MUNGU WAKO.**
**MIKA 6:8**

Haki, rehema na unyenyekevu ni mambo ambayo Mungu anayapenda. Hamu ya kufanya haki, kupenda rehema na roho ya kunyenyekea vinahitajika kwa ajili ya huduma ya urejesho.

Ni wajibu wetu kuingia katika shughuli ya kurejeza, kutoa muda wetu, upendo wetu na juhudi yetu ili kuokoa wale walio dhaifu na wanaopotoka.

**NDUGU ZANGU, IKIWA MTU WA KWENU AMEPOTELEA MBALI NA KWELI, NA MTU MWINGINE AKAMREJEZA, JUENI YA KUWA YEYE AMREJEZAYE MWENYE DHAMBI HATA ATOKE KATIKA NJIA YA UPOTEVU, ATAOKOA ROHO YA MAUTI, NA KUFUNIKA WINGI WA DHAMBI.**
**YAKOBO 5:19-20**

Wakati mwingine yatubidi hata kujihatarisha katika kuwaokoa wengine.

**HAKUNA ALIYE NA UPENDO MWINGI KULIKO HUU, WA MTU KUUTOA UHAI WAKE KWA AJILI YA RAFIKI ZAKE.**
**YOHANA 15:13**

Mchungaji anayemkimbia simba na kuacha kundi kuangamia yuko kama kibarua. Mchungaji mzuri hutoa uhai wake kwa ajili ya kundi.

**BASI IMETUPASA SISI TULIO NA NGUVU KUUCHUKUA UDHAIFU WAO WASIO NA NGUVU, WALA HAITUPASI KUJIPENDEZA WENYEWE.**
**WARUMI 15:1**

**MCHUKULIANE MIZIGO NA KUITIMIZA HIVYO SHERIA YA KRISTO.**
**WAGALATIA 6:2**

Inasemwa kuwa wakati mchungaji anapomwona kondoo akiwa mgonjwa anamweka kwenye mabega yake na kumpeleka katika zizi kwa kumlisha na kumtunza. Katika hali ya kumbeba huyo kondoo ile harufu ya ugonjwa inahama toka kwa kondoo na kwenda kwa mchungaji. Hatutegemei kuhusika katika kumrejesha ndugu aliyeanguka bila kuwa na hiari ya kudhurika na matatizo yake. Kurejesha siyo tu shauri la kuweka sheria; fanya hivi na utaweza kurudishwa. Urejesho unahusu kusahihisha na matunzo ambayo yaweza kutolewa kwa uvumilivu na upendo. Hata kama Hosea alivyolipa gharama ya kumkomboa mkewe, itatugharimu kitu fulani kumrejesha ndugu yetu. Tunachohitaji kukumbuka katika yote haya ni maneno ya Yesu.

**NA MFALME ATAJIBU, AKIWAAMBIA, AMINI, NAWAAMBIA, KADIRI MLIVYOMTENDEA MMOJAWAPO WA HAO NDUGU ZANGU WALIO WADOGO, MLINITENDEA MIMI.**

**MATHAYO 25:40**

Hakuna katika maandiko panaposema kuwa yule aliyeanguka atarejezwa kirahisi. Pamoja na uvumilivu kuugua kwingi na upendo tutahitaji hekima kutoka kwa Mungu ili kushughulika na mamzingara magumu ya dhambi.

**LAKINI HEKIMA ITOKAYO JUU, KWANZA NI SAFI, TENA NI YA AMANI, YA UPOLE, TAYARI KUSIKILIZA MANENO YA WATU, IMEJAA REHEMA NA MATUNDA MEMA, HAINA FITINA, HAINA UNAFIKI NA TUNDA LA HAKI HUPANDWA KATIKA AMANI NA WALE WAFANYAO AMANI.**
**YAKOBO 3:17-18**

Karibio lolote la kumshughulikia aliyeanguka lazima lifanywe kwa hekima iliyotajwa hapo juu. Ukatili na ulipizaji kisasi hauna nafasi katika hatua za uponyaji.

**TAFUTENI KWA BIDII KUWA NA AMANI NA WATU WOTE, NA HUO UTAKATIFU AMBAO HAPANA MTU ATAKAYEMWONA MUNGU ASIPOKUWA NAO.**
**WAEBRANIA 12:14**

Katika kufuata utakatifu baadhi wanaweza wakapoteza kuona kuwa Mungu anapenda tuishi katika amani pia. Hebu tusionekane kuwa tunapigana dhidi ya Mungu. Juhudi yoyote ya kuleta lawama haswa wakati mdhambi ameungama na kutubu ni upinzani wa wazi na kusudi la Mungu. Maandiko yanatuambia kuwa Shetani ni mshitaki wa ndugu, na kwamba tukifanya dhambi, tunaye wakili pamoja na Baba, Yesu Kristo mwenye haki ambaye ni mfunikaji wa dhambi zetu (Angalia Ufunuo 12:10 na I Yohana 2:1-1). Sasa vyote hivi vyaweza kuonekana kuwa tunachukua upande wa mkosaji. Katika nuru ya maandiko ya hapo juu hakuna njia nyingine ya kuchukua. Shetani akiwa anatushitaki na Yesu akitetea tutajiunga na upande upi?

Kule kutumia hekima, amani, rehema, upole n.k. katika kushughulika na mkosaji ni kujaribu kumwokoa. Bila kuungama na kutubu, hawezi kurejeshwa. Utaungama kwa mhukumu wako? Utakubali kujeruhiwa na kuwa dhaifu katika jeshi linalowapiga risasi majeruhi wake?

**UNGAMENI DHAMBI ZENU NINYI KWA NINYI, NA KUOMBEANA, MPATE KUPONYWA. KUOMBA KWAKE MWENYE HAKI KWAFAA SANA, AKIOMBA KWA BIDII.**
**YAKOBO 5:16**

Kama nikishindwa ninahitaji mtu wa kumwuungamia: mtu mwenye haki atakaye niombea ili kuponywa. Kama sina tegemeo la hisani na msaada, kuna haja gani kuungama? Ni asili ya kibinadamu kujaribu kuficha dhambi zetu. Dhambi ambazo hazijaungamwa huambukizwa na kusambaa. Wakati dhambi imefichwa kunakuwa na uharibifu zaidi kwa mtu binafsi na kanisa kwa ujumla. Jinsi rehema iliyozuiliwa, dhambi ina uwezekano wa kuto kuungamwa.

**MWONGOZO NA UTARATIBU:**

Kanuni za kushughulika na walioanguka na hatua zake zimeelezwa uwazi katika maandiko. Hatua hizi zitafuatwa kwa uangalifu ili tusizitukane nguvu kubwa ambazo Mungu

ameziweka kanisani.  Kiukweli sisi (kanisa) tumepewa uwezo wa maisha ya kiroho na kifo juu ya ndugu aliyeanguka.  Kwanza hebu tuangalie kanuni nyuma ya utaratibu.

**ANGALIENI MSIDHARAU MMOJAWAPO WA WADOGO HAWA, KWA MAANA NAWAAMBIA YA KWAMBA MALAIKA ZAO MBINGUNI SIKU ZOTE HUUTAZAMA USO WA BABA YANGU ALIYE MBINGUNI.  KWA MAANA MWANA WA ADAMU ALIKUJA KUKIOKOA KILICHOPOTEA.**
**MATHAYO 18:10-11**

Ukweli kwamba ndugu ameanguka haina maana kuwa siyo mtu muhimu kwa Mungu. Lazima tuwe waangalifu.  Inasemwa kuwa madaktari huzika makosa yao, na sisi tunapeleka yetu Jehanamu.

Bwana anaendelea kutoa mfano wa mchungaji aliyekwenda kumtafuta kondoo mmoja aliyepotea, na jinsi aliyefurahia alipomwona (Mathayo 18:12-13).   Mstari unaofuatia unaeleza kwa usahihi mapenzi na makusudi ya Bwana katika jambo hili.

**VIVYO HIVYO HAIPENDEZI MBELE YA BABA YENU ALIYE MBINGUNI KWAMBA MMOJA WA WADOGO HAWA APOTEE.**
**MATHAYO 18:14**

Baada ya kuonyesha kusudi, hebu sasa tuendelee na hatua za kushughulika na ndugu mkosaji.

**NA NDUGU YAKO AKIKUKOSA, ENENDA UKAMWONYE WEWE NA YEYE PEKE YENYE, AKISIKIA, UMEMPATA NDUGUYO.**
**MATHAYO  18:15**

Mtindo huu utazuia uharibifu ambao waweza kufanyika.  Kama ni muhimu kufanya jambo hilo lisifahamike hadharani basi hilo lifanywe.  Maandiko yanasema kuwa mahali ambapo hakuna mtoa habari ugomvi hupungua.  Haswa katika mashauri yenye ugomvi ni vyema kushughulika nayo kwa faragha.  Matokeo ya kueneza hilo jambo ili kila mtu ajue yaweza kuwa na maafa, haswa kwa kuwa mambo ya kanisa yanaweza kuwana njia ya kutokea nje.  Hii ni lawama.

Mbinu hii haimgoji mkosaji mkosaji kufanya hatua yake ya kwanza.  Inatoa kwake kila huruma na kufikiria nafasi ya toba na upatanisho.  Haimhukumu isivyopasa kuwa ni mwenye hatia.  Inampa tumaini.  Kama ndugu mkosaji hatubu, basi utaratibu uendelee.

**LA, KAMA HASIKII, CHUKUA PAMOJA NAWE TENA MTU MMOJA, AU WAWILI ILI KWA VINYWA VYA MASHAHIDI WAWILI AU WATATU KILA NENO LITHIBITIKE.**
**MATHAYO  18:16**

Mbnu hii inaendelea bila jambo hilo kufanywa wazi hadharani kukiwa na mashahidi wa kuthibitisha ili kuonyesha jinsi jambo lilivyo nzito huku pande zote mbili zikilindwa.  Hii pia inamlinda mtu kutokana na mashitaka ya uongo yakitolewa hadharani.

Pia ifahamike kuwa mashitaka dhidi ya mzee lazima yasikilizwe na mashahidi wawili au watatu.  Viongozi mara nyingi hufanyiwa tuhuma za uongo na ni shauri lenye hekima

(I Timotheo 5:19).  Kama karibio hili la huruma halipokelewi, basi hakuna uchaguzi bali kufikisha jambo hili kwa mbele ya kanisa.

**NA ASIPOWASIKILIZA WAO, LIAMBIE KANISA, NA ASIPOSIKILIZA YA KANISA PIA, NA AWE KWAKO KAMA MTU WA MATAIFA NA MTOZA USHURU.  AMINI NAWAAMBIENI, YOYOTE MTAKAYOFUNGA DUNIANI YATAKUWA YAMEFUNWA MBINGUNI, NA YOYOTE MTAKAYOFUNGUA DUNIANI YATAKUWA WAMEFUNGULIWA MBINGUNI.**
**MATHAYO 18:17-18**

Mamlaka ya kuogofya ya kanisa ni ile iliyowekwa katika swala la kumhukumu mwenye dhambi. asiyetubu.  Sasa neno la Mathayo 18:15 litaonekana kueleza kuwa jambo hili linaonekana shauri hili linahusu washirika wawili wa kanisa.  Hata hivyo hatua za rehema na utaratibu uliotumika unaweza ukawa kama mfano kwa mashauri mengine.

Jambo la kushughulika na dhambi katika kanisa limetajwa katika Wakorintho wa kwanza na pili, Wathesalonike wa pili na pia katika Timotheo wa kwanza.  Makaribio haya tofauti yanatuonyesha kuwa Mungu amelipa kanisa mamlaka na uhuru wa kushughulika na dhambi katika hali mbali mbali.

**WAHURUMIENI WENGINE WALIO NA SHAKA, NA WENGINE WAOKOENI KWA KUWANYAKUA KATIKA MOTO.  NA WENGINE WAHURUMIENI KWA HOFU, MKICHUKIA HATA VAZI LILIOTIWA UCHAFU NA MWILI.**
**YUDA 22-23**

Hii siyo kushauri  kwa upendeleo.  Ukweli Neno la Mungu linatuambia kama sisi tunapendelea watu tunafanya dhambi.  Kama tukiruhusu wengine wasamehewe kwa jinsi walivyo na wengine kuadhibiwa kwa kosa hilo hilo tunafanya dhambi na kutenda tendo la ukatili mbele za Mungu na kanisa.  Yafuatayo ni orodha ya maandiko yanayoeleza jinsi ya kushughulika na dhambi kanisani.

**NA IKIWA MTU AWAYE YOTOTE HALISHIKI NENO LETU LA WARAKA HUU, JIHADHARINI NA MTU HUYO, WALA MSIZUNGUMZE NAYE, APATE KUTAHAYARI LAKINI MSIMHESABU KAMA ADUI, BALI MWONYENI KAMA NDUGU.**
**2 WATHESALONIKE 3:14-15**

**SASA NAWASIHI NDUGU, WAWEKENI ALAMA WALE WALELTAO MGAWANYIKO NA KUPOTOSHA MAFUNDISHO YALE MLIOJIFUNZA, WAEPUKENI.**
**WARUMI 16:17**

**KUMTOLEA SHETANI MTU HUYO, ILI MWILI UADHIBIWE ILI NA ROHO IOKOLEWE KATIKA SIKU YA BWANA YESU.**
**I WAKORINTHO  5:5**

**KATIKA HAO WAMO HIMENAYO NA ISKANDA, AMBAO NIMEMPA SHETANI, WATU HAO ILI WAFUNDISHWE WASIMTUKANE MUNGU.**
**I TIMOTHEO 1:20**

**WALE WADUMUO KUTENDA DHAMBI UWAKEMEE MBELE YA WOTE, ILI NA WENGINE WAOGOPE.**

**I TIMOTHEO 5:20**

**YAMTOSHA MTU WA NAMNA HII ADHABU ILE ALIYOPEWA NA WALIO WENGI, HATA KINYUME CHA HAYO, NI AFADHALI MSAMEHE NA KUMFARIJI, MTU KAMA HUYO ASIJE AKAMEZWA KATIKA HUZUNI YAKE IPITAYO KIASI.**
**2 WAKORINTHO 2:6-7**

Kutokana na maandiko hayo tunaweza kuona matumizi ya kukemea, kutenga na ushirika na kumtoa mtu kwa shetani ili mateso yalete toba. Matumizi ya hatua za namna hiyo yafanywe kwa maombi na bila woga, na tegemeo la upatanisho na urejesho liwe siku zote akilini.

## WENYE KUANGALIA AMBAO NI WAAMINIFU:

Jambo moja ambalo mara nyingi haliangaliwi vyema ni wale wahusika wasio na hatia na dhambi. Mara nyingine wana familia au washirika wengine wanapata taabu kwa ajili ya mdhambi mmoja ambaye hakutubu ingawaje hawana hatia. Kuyapuuza mahitaji ya watu hawa ambao wanaumia bila kuwa na makosa ni ukatili na haiko kama Kristo hata kidogo. Tunaposhindwa kuwafikilia watu hawa wanaoumia, tunakosa upendo na kuwaweka hawa katika hatari ya kuwa na uchungu. Kuna maumivu na uchungu wa kutosha ulimwenguni bila ya mbegu ya hivi kupandwa kanisani. Tusiulize swali juu ya uaminifu wao na kuogopa kuwa tutafaidika kwa hivi vitu tukikosea, wacha iwe kwa sababu tuna rehema.